TAARIFA YA MKURUNGEZI WA JIJI LA DAR ES SALAAM KWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS-TAMISEMI, MHESHIMIWA SULEIMANI JAFFO (MB), KUHUSU MPANGO WA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM WA KUENDELEZA UTALII KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM

17 MACHI, 2018

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Suleimani Jaffo(Mb),

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mheshimiwa Paul Makonda,

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Mheshimiwa Sophia Mjema,

Mstahiki Meya wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita Charles,

Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam, Bi. Theresia Mmbando,

Wakurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Kinondoni, Temeke, Ubungo, Kigamboni

Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Jiji,

Wageni waalikwa,

Ndugu wananchi,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana,

1.0 UTANGULIZI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, uzima na kutuwezesha kukutana leo. Ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mgeni Rasmi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mheshimiwa Suleimani Jaffo (Mb), kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi wa shughuli za kukuza na kuutangaza utalii katika Jiji la Dare s Salaam. Halmashauri ya Jiji imeanza kushughulikia suala la kukuza utalii Dar es

Salaam ikiwa ni sehemu ya hatua za utekelezaji wa mpango wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wa kuendeleza utalii katika Jiji hilo.

Jiji la Dar es Salaam ni maarufu kisiasa, kibiashara na ina vivutio vingi vya utalii kama vile majengo na maeneo ya kihistoria, fukwe, bandari na visiwa, sehemu za kitamaduni, vifaa na kazi za asili, bustani na maeneo ya wazi na misitu. Aidha, Jiji hili ni kiunganishi cha miundombinu kati ya mikoa na nchi za jirani kwa kuwa na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Bandari, Kituo Kikubwa cha Mabasi na Reli.

Miundombinu hiyo ya usafiri inasaidia kwa kiasi kikubwa kuvifikia vivutio vingine vingi vikubwa vya utalii vilivyopo katika miji mingine kama vile mji wa kihistoria wa Bagamoyo, magofu ya Kilwa, mbuga za wanyama za Mikumi, Saadani, Serengeti, kisiwa cha Zanzibar na Mlima Kilimanjaro.

2.0: MPANGO WA KUKUZA UTALII

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa kuzingatia hilo, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam iliazimia kukuza na kuimarisha shughuli za utalii katika Jiji kwa kuanzisha Dawati la Utalii mwaka 2008 na shughuli za utalii ziliingizwa rasmi kwenye bajeti ya Halmashauri ya Jiji kuanzia kipindi hicho. Aidha, Halmashauri ilizingatia maoni na ushauri uliotolewa na wadau mbalimbali kupitia mikutano ya wadau iliyoonesha fursa ambayo Jiji la Dar es Salaam inazo na umuhimu wa kulifanya Jiji hili kuwa kitovu cha utalii. Fursa hizo zilichochea Halmashauri ya Jiji kujikita rasmi kwenye kukuza utalii wa mijini na kuongeza mapato ya Halmashauri.

3.0 LENGO LA HALMASHAURI

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mpango wa Halmashauri wa uendelezaji utalii jijini unalenga kubadili sura ya Jiji kutoka kuwa njia ya kupita wageni (transit hub) na kuwa kituo cha utalii (tourists destination) na kuongeza muda wa wageni kukaa jijini ili kuongeza mapato ya Jiji.

Hali halisi ya sasa ni kwamba idadi kubwa ya wageni na watalii wafikao nchini hutumia Bandari na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kwenda kwenye vivutio vingine vya utalii kama vile Ngorongoro, Serengeti, Zanzibar na sehemu nyingine nyingi za nchi na kushindwa kujua kama Dar es Salaam ina sehemu ambazo watalii wanaweza kukaa kabla ya kuendelea na safari zao, na hiyo ni sababu iliyofanya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kuamua kuendeleza na kuvitangaza vivutio vya utalii vilivyoko jijini.

4.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA UENDELEZAJI UTALII

4.1: KAZI ZILIZOKWISHAFANYIKA

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Shughuli mbalimbali zilizokwishafanyika za kuendeleza utalii ni kama zifuatazo:-

- Uhifadhi wa majengo ya kihistoria kama moja ya kivutio kikubwa kwa wageni hasa wa Kijerumani kwa kuweka nembo maalum kwenye majengo hayo ili kuyatangaza. Majengo yaliyowekewa nembo hizo ni pamoja na Jengo la Halmshauri ya Jiji (City Hall), Kanisa Kuu la Mt. Josefu, Kanisa la Azania Front, Ukumbi wa Karimjee na jengo la Old Boma.

- Kuanzisha Kitabu cha Utalii kinachotoa taarifa mbalimbali ya vivutio, mahali pa kwenda, vitu muhimu vya kuangalia na taarifa za kiusalama ili kumrahisishia mgeni anapotembelea sehemu mbalimbali jijini. Kitabu hicho kiko kwenye mahoteli, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere na baadhi ya maeneo ya kitalii.

- Kuanzisha Dawati la Utalii kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambalo linalotoa taarifa mbalimbali za kitalii Jijini kama vile maeneo ya kutembelea, mahoteli, migahawa, vyombo vya usafiri na gharama zake na taarifa mbalimbali za vivutio vingine nchini.

- Kuendelea kutangaza vivutio vya utalii vya Jiji la Dar es Salaam ndani na nje ya nchi kwa kushirikiana na sekta binafsi na Bodi ya Utalii ya Dar es Salaam.

- Kwa udhamini wa UNESCO tumeainisha vikundi vya sanaa za kitamaduni zilizoko Jijini na kuona jinsi ya kuwajengea uwezo ili waweze kuuza kwenye soko la kimataifa.

- Kushirikisha wadau mbalimbali katika zoezi la kutangaza vivutio vya utalii Jijini.

- Kufanya "survey" ya utalii ili kujua mwelekeo wa sekta kwa watalii waliofika Dar es Salaam (Tourists Exit Survey Report).

- Uchapishaji wa Ramani za Utalii za Dar es Salaam zinazoonesha vivutio na mahali vilipo.

- Kutoa mafunzo kwa waongoza utalii (Tour Guides) watakaotumika kuongoza wageni na watalii watakaotoa taarifa sahihi za vivutio, historia ya Mji wakati wa kuwatembeza watalii kwenye vivutio mbalimbali.

4.2: KAZI ZINAZOENDELEA KUFANYIKA

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inaendelea kufanya kazi kubwa zaidi ya kufanikisha lengo lake la kuendeleza utalini Jijini kwa kufanya kazi zifuatazo:

- **UHIFADHI WA MAJENGO**

Katika mradi wa uhifadhi majengo ya kihistoria ambao ni moja ya vivutio vikubwa vya watalii, kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wabunifu wa Majengo Tanzania, umefanyika

ukarabati wa jengo la Old Boma ambalo kihistoria lilijengwa na Sultani mwaka 1860 na kumaliziwa na Wajerumani mnamo mwaka 1900. Jengo hili lilikarabatiwa kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya (European Union) kupitia wadau wa Halmashauri ambao ni Jumuiya ya Wabunifu Majengo Tanzania.

Katika jengo hilo, Halmashauri imeanzisha Kituo Maalum cha Utalii, "One Stop Tourism Centre," ambacho huduma mbalimbali za kiutalii zitakuwa zikitolewa katika jengo hilo la kale la Old Boma. Baadhi ya huduma zitakazotolewa ni mgahawa wa kiutalii, maduka ya kitalii, ukumbi mdogo wa mikutano, dawati la kutolea taarifa za kitalii pamoja na makumbusho ya mji.

- **MGAHAWA WA KISASA WA KITALII**

Mgahawa wa kisasa wa kitalii utakuwa katika eneo la juu la jengo ambako kuna uwazi ambao turubai mahsusi linatarajiwa kuwekwa hivi karibuni ili kutoa kivuli na kuvutia wateja. Turubai hilo la kisasa limetengenezwa nchini Ujerumani kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

Halmashauri ya Jiji imechangia gharama za kupima uwezo na ubora wa turubai hilo kupitia Wakala wa Viwango nchini (TBS) na gharama za kulitoa bandarini zitachangiwa na Halmashauri ya Jiji.

- **MAKUMBUSHO "CITY MUSEUM"**

Makumbusho hayo yameshaanza kazi kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wabunifu Majengo Tanzania. Watalii wa ndani na nje wanafika kwenye maonyesho ambayo yapo katika ghorofa ya pili kujionea historia mbalimbali za Jiji la Dar es Salaam iliyopo kabla ya wakoloni, nyumba za asili za Waafrika, Waarabu, Wajerumani, Wahindi na hali ilivyo hivi sasa.

- **MADUKA YA KITALII**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika jengo la Old Boma kuna maduka mawili ya kitalii (Curio shops) ambayo hutoa huduma mbalimbali kwa watalii wa ndani na nje ya nchi pamoja na wananchi.

- **DAWATI LA MAELEZO KWA WATALII**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wasanifu Majengo Tanzania ndani ya jengo la Old Boma tumeweka Dawati la Maelezo kwa watalii wa ndani na nje ya nchi ambako watalii wanapata taarifa mbalimbli za Jiji zikiwemo ramani zinazonesha sehemu muhimu za Jiji kama vile mahoteli, vivutio vya kitalii, usafiri, fukwe na sehemu mbalimbali za vivutio.

- **MABASI YA KUTEMBEZA WATALII**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashauri ya Jiji imeanzisha mradi wa mabasi ya kitalii kwa lengo la kuwasafirisha na kuwatembeza watalii kwenye vivutio mbalimbali vya kitalii vilivyoko Dar es Salaam na miji ya karibu. Kazi hii itaiongezea mapato Halmashauri na pia itakuza taswira ya Jiji la Dar es salaam na kuitangaza nchi yetu sehemu mbalimbali. Katika hilo, shughuli zilizofanyika mpaka sasa ni kwamba basi moja la kuhudumia watalii limeshawasili na limeshaanza kazi rasmi na Serikali imeshatoa kibali cha kununua basi la pili.

- **VIPEPERUSHI**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashauri ya Jiji imeandaa na kusambaza sehemu mbalimbali vipeperushi vyenye maelezo sehemu za vivutio vya utalii na njia za kuelekea sehemu hizo. Vipeperushi hivyo vinaonesha njia basi linapopita, muda na gharama zake.

- **MAFUNZO YA KUJENGA UELEWA WA KUHUDUMIA WATALII**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashuri ya Jiji imepanga kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wanaotoa huduma kwa watalii kama madereva wa teksi 25 wanaoegesha kwenye mahoteli, eneo la karibu na bandari ya meli na boti zinazotoka visiwa vya Unguja na Pemba na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Madhumuni ya mafunzo haya ni kuongeza ujuzi wao ili kuhakikisha wanatoa huduma inayokidhi matarajio ya mtalii pamoja na kuelewa umuhimu wa sehemu tofauti za vivutio.

Pamoja na madereva wa teksi Halmashauri ya Jiji imepanga kutoa mafunzo kwa mama lishe 25. Madhumuni ya mafunzo haya ni kuboresha, kuimarisha ujuzi wa watoa huduma ya chakula na vinywaji katika kufikia viwango vya kimataifa ili kutoa huduma bora kwa wageni wa nje na ndani ikiwemo vyakula vya asili vya Tanzania. Mafunzo haya ya wiki moja yatatolewa na Chuo cha Taifa cha Utalii.

- **KUTANGAZA UTALII NDANI NA NJE YA NCHI**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika kuutangaza utalii wa Dar es Salaam, Halmashauri ya Jiji imetengeneza "documentary" ya utalii ya Jiji la Dar es Salaam ambayo imekamilika. "Documentary" hii ina nia ya kulitangaza Jiji la Dar es Salaam ndani na nje ya nchi pamoja na vivutio vyake vya kitalii.

5.0: KUTENGENEZA MAZINGIRA MAZURI KWA WATALII

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika hili Halmashauri imepanga:

- Kuendeleza maeneo ya bustani za kupumzikia (City Park), sehemu ya kuchezea watoto na sehemu ya ngoma za asili katika eneo la Halmashauri la DRIMP

ambapo kwa sasa Halmashauri imeshaanza kazi ya kutengeneza bustani, sehemu ya kuchezea watoto na kuchezea ngoma za jadi.

- Kuendeleza eneo la viwanda vidogo vidogo eneo la Mwananyamala na Gongo la Mboto ambako baadhi ya vikundi hutengeneza bidhaa ambazo hupendwa na watalii, bidhaa hizo ni kama hereni, bangili, vikapu na mabatiki ambayo huvaa au kuchukua kama zawadi kupeleka makwao.

6.0: MIPANGO INAYOFUATA

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashauri ya Jiji imepanga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuendeleza Dawati la Utalii kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere linalotoa taarifa mbalimbali za kitalii jijini kama maeneo ya kutembelea, mahoteli, migahawa, vyombo vya usafiri na gharama zake na taarifa mbalimbali za vivutio vingine nchini.

- Kuendelea kutafuta miradi mingine ya utalii kama vile "tourism village", "amusement parks", kuendelea kununua mabasi mengine ya yatakayotoa huduma ya usafiri kwa watalii na wananchi, magari madogo na "luxurious" bajaji, kuendeleza bustani na kuendelea kushirikiana na wadau wengine kuongeza watalii jijini.

- Kuanzisha matamasha ya Kitaifa (Events & Festivals) yatakayosaidia kutangaza Jiji na kuleta idadi kubwa ya watalii kama ilivyo Sauti za Busara Zanzibar.

- Kuamsha uelewa wa wananchi juu ya vivutio vya utalii vilivyoko jijini kwa kuwa na siku ya kusafisha fukwe za Jiji la Dar es Salaam. Tayari Halmashauri

ilishajaribu kufanya hivyo mara mbili, tarehe 17 Januari, 2009 na tarehe 19 Februari, 2011 ikiwa na Kaulimbiu "*Furahia fukwe safi, kukuza utalii Dar".*

- Uwekezaji kwenye jengo la Old Boma, kama chanzo kikubwa cha mapato na ajira kwa wananchi wa Dar es Salaam.

- Kuanzisha safari za boti kwenda visiwa vya Bongoyo na Mbudya.

- Kuendeleza bustani ya Karimjee, Drimp na Old Boma ili iweze kuvutia zaidi.

7.0: HITIMISHO

Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Halmashauri ya Jiji inathamini mchango mkubwa wa wadau katika sekta ya utalii na tutaendelea kushirikiana nao katika hatua zote za utekelezaji wa mpango wa Halmashauri wa kukuza utalii katika Jiji la Dar es Salaam.
Tumeanza vizuri na tutaendelea kuunga mkono kwa vitendo juhudi za Serikali za kuendeleza utalii nchini.

Naomba kuwasilisha,

SIPORA J. LIANA
MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM